



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA



Tafadhalni unapojibu taja :-

Kumb. Na.MDC/L.10/7/VOL.IV/48

31/07/2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba anakaribisha maombi ya kazi kwa watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi moja (1) ya **Mwandishi Mwendesha Ofisi II**. Tangazo hili ni kutokana na Kibali cha Ajira mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye Kumb. Na. FA.170/361/01“B”/72 cha tarehe 22 Juni, 2023. Mchanganuo wa nafasi hiyo ni kama inayoonekana hapa chini:-

1. MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II (NAFASI 01)

1.1. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne au Sita mwenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha NTA level 6 ya Uhazili
- ii. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno Mia Moja (100) kwa dakika moja.
- iii. Awe amepata mafunzo ya programu za Komputa za Ofisi kama vile; Word, Excel, Power point, internet, E-Mail na Publisher kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.2. KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kuchapa barua, Taarifa na Nyaraka za kawaida na za Siri;
- ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa;
- iii. Kutunza Taarifa za kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi nyingine;
- iv. Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa wa majukumu ya kazi;

- v. Kupokea majalada na kusambaza kwa Maofisa walio katika Divisheni/Kitengo/Sehemu husika.
- vi. Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika.
- vii. Kupanga dondo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali na
- viii. Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya Ofisi.

1.3. NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara ni kwa Mujibu wa viwango vya Mishahara ya Serikali yaani **TGS C** kwa mwezi.

1.4. MASHARTI YA AJIRA

Masharti ya Ajira hii ni Ajira ya Kudumu na Malipo ya Pensheni.

1.5. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA MWOMBALI


- i. Waombaji wawe Raia wa Tanzania wenye umri usiopungua miaka Kumi na Nane (18) na usiozidi miaka Arobaini na Tano (45).
- ii. Waombaji waambatanishe cheti cha kuzaliwa
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed **(CV)**) yenye anwani na Namba za Simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Waombaji waambatanishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) wasio na Kitambulisho cha Taifa waandike Namba ya NIDA.
- v. Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya Taaluma, Vyeti vya Kidato cha Nne (Form IV) au Kidato cha Sita (Form IV na Form VI) na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- vi. Picha Mbili 2 (**passport size**) za rangi za hivi karibuni ziandikwe jina kwa nyuma.
- vii. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganishi na Mamlaka husika (**TCU**) na (**NACTE**) na taarifa ya ulinganishi iambatishwe kwenye maombi
- viii. **Testimonials Provisional Result, Statement of Result“ na Hati za Matokeo (Result Slip) HAVITAKUBALIWA**
- ix. Waombaji wa kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia waliopo katika

Utumishi wa Umma wasiombe kazi na wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyo
katika Waraka CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.

- x. Uwasilishwaji wa Taarifa na Sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.
- xi. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba kabla au ifikapo **tarehe 14 Agosti, 2023** saa 9:30 alasiri.

Barua za maombi zitumwe kwa anwani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba
S.L.P 263,
IFAKARA.**


Eng. Stephano B. Kaliwa,
MKURUGENZI MTENDAJI (W),
MLIMBA.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MLIMBA

Nakala: - Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
Jengo la Utumishi (UDOM) na
Eneo la Dkt. Asha Rose Migiro
S.L.P 2320
DODOMA.

- Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba
www.mlimbadc.go.tz
- Mbao za matangazo